## COUNTY GOVERNMENT OF LAMU

## THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

## THE HANSARD

**Thursday 4th June, 2026**

*The Assembly met at the*

*Main Chambers, at 2:30 p.m.*

[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

### PRAYERS

**[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Next Order.

**Clerk-at-the-Table**: Statements.

### STATEMENT/QUESTIONS

*UPUNGUFU WA MAJI MATONDONI, WADI YA MKOMANI*

**MCA Somoe Abulrahman Mahmoud (*Nominated*):** Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu 41(2c) kuomba taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati husika ya Ardhi na Maliasili kuhusu tatizo la muda mrefu la upungufu wa maji katika eneo la Matondoni. Wadi va Mkomani

Mheshimiwa Spika, Matondoni ni mojawapo ya vijiji vikubwa katika Kisiwa cha Lamu, ikiwa na wakazi zaidi va 2.500 ambao wanategemea hasa visima vifupi, uvunaji wa maji ya mvua na huduma ndogo ya maji ya bomba kwa matumizi ya nyumbani. Kwa miezi kadhaa iliyopita, wakazi wamekabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana na kukauka kwa visima, kuharibika mara kwa mara

***Disclaimer**: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

kwa mfumo wa maji ya bomba, na kuongezeka kwa chumvi katika vyanzo vya maji ya chini ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ninaomba taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati husika ya Ardhi Maliasili kuhusu mambo yafuatayo:

1. Hali ya sasa ya upatikanaji wa maji katika Matondoni ni ipi?
2. Ni hatua gani zimechukuliwa kurekebisha mfumo uliopo wa maji ya bomba?
3. Ni hatua gani za muda mfupi zimepangwa ili kukabiliana na tatizo hili?
4. Kiasi gani cha fedha kimetengwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ya miradi ya maji katika Matondoni?

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Matondon hawawezi kuendelea kuteseka kimya kimya huku haki ya kikatiba ya kupata maji safi na salama chini ya Ibara ya 43(1)(d) ikivunjwa.

Asante.

**MCA Husuni Alawi Mohamed (*Nominated*):** Asante Bwana Spika, naomba nipewe muda wa siku kumi ili kuleta majibu katika bunge hili.

**The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Mheshimiwa Somoe uko sawa na huo muda?

**MCA Somoe Abdulrahman Mahmoud (*Nominated*):** Nimeridhika Bwana Naibu Spika.

**[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Next Order.

**Clerk-at-the-Table**: Motion.

***Disclaimer**: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

**MOTION**

*APPROVAL OF COUNCIL MEMBERS FOR VOCATIONAL TRAINING CENTRES (FORMER YOUTH POLYTECHNIC)*

**MCA Mohamed Aboud Abubakar (*Faza*):** Thank you Mr Deputy Speaker.

Mr. Deputy Speaker Sir, I differ this motion to the next sitting.

**[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** You are in order Honorable Simba and your request is granted.

*ADJOURNMENT*

**[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until next week Tuesday, 9th June, 2026 at 2:30 p.m.

***The Assembly rose at 3:15 p.m.***

***Disclaimer****: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

***Disclaimer**: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*